**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

## TAARIFA KWA UMMA

Ninasikitika kutangaza kifo cha kwanza cha mgonjwa wa COVID-19 (ambukizo la virusi vya corona) hapa nchini kilichotokea alfajiri ya leo tarehe 31 Machi 2020 katika kituo cha matibabu ya wagonjwa wa COVID-19 kilichopo Mloganzila, Dar es Salaam.

Marehemu ni Mtanzania, mwanaume mwenye umri wa miaka 49 ambaye pia alikuwa akisumbuliwa na maradhi mengine.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi, na tunatoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu.

Hadi kufikia leo asubuhi tarehe 31 Machi, 2020 jumla ya watu waliopata maambukizi ya COVID-19 nchini ni 19, aliyepona mmoja (1) na kifo kimoja (1).

**Ummy A Mwalimu (Mb)**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**
**31.03.2020**